

**KWENDA: MWENYEKITI, KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**KUTOKA: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

TAREHE: 7 Machi, 2022

**YAH: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA
MWEZI FEBRUARI, 2022.**

A: MAPATO:

**I. VYANZO VYA MAPATO YA NDANI VYA HALMASHAURI (OWN
SOURCES)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022, Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilijiwekea lengo la kukusanya mapato ya **Tzs 9,106,108,000**. Kwa kipindi cha mwezi Februari, 2022 zimekusanywa **Tzs 493,240,531.42** sawa na asilimia **5.42** ya Lengo kwa Mwaka. Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari 2022 imeweza kukusanya Jumla ya **Tzs 5,990,945,994.85** sawa na asilimia **65.79** ya lengo la mwaka.

Taarifa mlingano ya mwezi Februari, 2022

Lengo la Halmashauri kwa mwezi Februari, 2022 ni kukusanya kiasi cha **Tzs 758,842,333.31** ambapo zimekusanywa **Tzs 493,240,531.42** sawa na asilimia **65.00** ya lengo la mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatao ni mchanganuo wa mlingano wa

Mapato halisi kwa mwezi Februari, 2022 kama yalivyokusanywa.

Jedwali la Mlingano: Januari 2022- Februari 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pun gufu,	(%)
1	Januari	758,842,333.51	1,061,335,474.48	302,493,141.17	139.86
2	Februari	758,842,333.51	493,240,531.42	(265,601,801.89)	65.00

Upungufu wa ukusanyaji kwa mwezi Februari 2022 umetokana na ukweli kuwa, ni mwezi wa makusanyo ya chini (low season).

II RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilikisia kupokea Ruzuku kutoka Serikali Kuu jumla ya **Tzs 32,818,771,000.00**. Kwa mwezi Februari, 2022 fedha zilizopokelewa ni **Tzs 2,269,010,733.87** sawa na asilimia **6.92** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha Halmashauri ilitarajia kupokea jumla ya **Tzs 2,734,897,583.33** kwa mwezi, ambapo kiasi kilichopokelewa ni **Tzs 2,269,010,733.87** sawa na asilimia **82.97** ya makisio ya mwezi; Aidha halmashauri katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari, 2022 imeweza kupokea Ruzuku toka Serikali Kuu Jumla ya **Tzs 18,222,014,602.91** sawa na asilimia **55.52** ya lengo la mwaka.

Ruzuku iliyopokelewa kwa mwezi Februari, 2022 ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

JUMLA YA MAPATO YA RUZUKU: Januari 2022-Februari 2022

Na	Mwezi	Makisio	Mapato halisi	Ongezeko/Pungufu,	(%)
1	Januari	2,734,897,583.33	2,215,332,449.68	(519,565,183.65)	81.00
2	Februari	2,734,897,583.33	2,269,010,733.87	(465,886,849.46)	82.97

Fedha za ruzuku zilizopokelewa ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari, MDH. Fedha zilizopokelewa nje ya bajeti ni;

Tzs 40,000,000.00 kutoka TEA kwa ajili ya ukarabati shule ya msingi Gomvu.

Tzs 11,320,000.00 kutoka TASAF kwa ajili ya mafunzo kwa walengwa jinsi ya kuweka akiba.

B: MATUMIZI:

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni 2022 Halmashauri imekisia kutumia **Tzs. 41,924,878,999.76** kati ya fedha hizo **Tzs 32,818,771,000.00** ni kwenye maeneo ya Ruzuku; na **Tzs. 9,106,108,000.00** ni katika maeneo yasiyo ya Ruzuku.

Matumizi halisi kwa mwezi Februari 2022, ni **Tzs 2,988,520,885.63** sawa na asilimia **7.13** ya bajeti yote ya matumizi ya mwaka. Aidha matumizi ya ruzuku kwa

Mwezi Februari, 2022 ni Tzs 2,303,001,541.23 sawa na asilimia 7.02 ya bajeti ya mwaka.

Matumizi ya vyanzo vya ndani kwa mwezi Februari, 2022 ni Tzs 685,519,344.40 sawa na asilimia 7.53 ya bajeti ya mwaka.

Aidha Halmashauri kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Februari, 2022 imeweza kutumia jumla ya Tzs 21,926,916,646.01 sawa na asilimia 52.30 ya lengo la mwaka.

Mchanganuo wa matumizi ya Fedha Mwezi Februari, 2022 ni kama ifuatavyo:

▪ Matumizi maeneo yasiyo ya ruzuku	Tzs	685,519,344.40
▪ Matumizi maeneo ya Ruzuku	Tzs	2,303,001,541.23
Jumla	Tzs	2,988,520,885.63

Matumizi yaliyofanyika ni katika maeneo ya mishahara, ruzuku ya matumizi ya kawaida, elimu bila malipo kwa elimu msingi na sekondari, MDH, TASAF, Mfuko wa pamoja wa Afya (Basket fund) na matumizi ya vyanzo vya mapato ya ndani.

Matumizi ya fedha zilizopokelewa nje ya bajeti kwa mwezi Februari 2022 ni;

Tzs 2,280,000.00 kwa ajili ya shughuli za uratibu wa chanjo ya UVIKO 19.

Tzs 11,320,000.00 kwa ajili ya mafunzo kwa walengwa jinsi ya kuweka akiba.

Aidha kuna fedha zilizopokelewa mwezi Oktoba kutokana na tozo za miamala kutoka Serikali kuu Tzs 250,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya mtaa wa kichangani kata ya Somangila, fedha hizo zimehamishiwa akaunti ya maendeleo ya kata Somangila kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Jedwali "A", "B" "C" na "D" ikionyesha muhtasari Mapato, Matumizi, mchanganuo wa taarifa mlingano wa mapato ya ndani wa mwezi Februari, 2022 na mchanganuo wa matumizi (itemized),

Nawasilisha,

Mwamtobe U.E
**K.N.Y: MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**